BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Tano – Tarehe 13 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali Kuu.
(b) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
(c) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea.
(d) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Miradi ya Maendeleo.
(e) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA.
(f) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi Maalum (Special Audit).

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Kamati ya PAC kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali Kuu.
(b) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Miradi ya Maendeleo.
(c) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi Maalum (Special Audit).

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
(b) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma na taasisi zinazojitegemea.
(c) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

21. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Katika kukabiliana na wimbi la biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikiwakamata na

kuwashitaki wahamiaji hao haramu na baadae kufungwa au kupigwa faini. Aidha, wahamiaji wanaofungwa mara kwa mara baada ya kumaliza kifungo chao, wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la kuchelewa kurejeshwa katika nchi zao za asili, hivyo kubakia kwenye magereza kwa upande wa Tanzania Bara na Vyuo vya Mafunzo kwa upande wa Zanzibar. Hali hii husababisha magereza na Vyuo cha Mafunzo kuendelea kuhudumia malazi, matibabu na chakula.

(a) Kwa kuwa Idara ya Uhamiaji ndiyo inayohusika na uhamiaji huo, kwa nini Idara hiyo isitoe fungu la kuwahudumia wahamiaji hao haramu baada ya kumaliza vifungo vyao.

(b) Kwa upande wa Zanzibar, kuna wafungwa wangapi ambao wamefungwa kwa kuingia nchini kinyume na sheria.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

38. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika baadhi ya njia za ndani za maeneo mbali mbali Zanzibar, zina changamoto kubwa ya kutokuwa na mitaro, hali inayopelekea kutuwama kwa maji machafu wakati wa mvua. Mfano wa maeneo hayo ni Shehia ya Kiembesamaki, Shehia ya Mombasa, Shehia ya Mchina Mombasa na baadhi ya maeneo mengine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitatua kadhia hiyo ikizingatiwa kuwa, wananchi wanazitegemea njia hizo kwa matumizi tofauti ya kijamii na kiuchumi.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

60. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa timu za mpira wa miguu za Zanzibar kama vile JKU, Magereza, Small simba na Malindi zimekuwa zikifanya vibaya kwenye ligi za ndani na nje ya nchi kutokana na kukosa wawekezaji kama ilivyo kwa timu za Tanzania Bara. Na kwakuwa wawekezaji wa timu nyingi za Ulaya kama vile

Manchester City, Liver pool na Manchester United hutoka nje ya nchi ya Uingereza (Arabuni).

Je, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itawashawishi matajiri wa nje kuja kuwekeza kwenye timu zetu za Zanzibar ili tuweze kuinua soka la nchi hii.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

81. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya awamu ya nane imo katika hatua mbali mbali za kuwaondolea kero wananchi wake kwa kuwajengea miradi mbali mbali ya kimaendeleo. Wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, wako wananchi masikini ambao hutoa ardhi zao pamoja na miti ya aina mbali mbali kupisha miradi hiyo na mara nyingi kulipwa fidia. Hata hivyo, kwa vile bei elekezi zilifanyiwa marekebisho tokea mwaka 2020, fidia hizo si za kuridhisha kulingana na mfumko wa bei na kushuka thamani ya sarafu.

(a) Je, ni lini Serikali itaziboresha bei elekezi hizo zilizopo tokea mwaka 2020.

(b) Je,Serikali inatumia vigezo vipi kuziongeza bei hizo elekezi ili kuendana na wakati.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

24. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na wimbi la wizi wa miundombinu ya barabara na maji na kuitia Serikali hasara kubwa na kurejesha nyuma juhudi zake za kuwaletea maendeleo wananchi.

(a) Kwa kuwa wizi huo unahusishwa na biashara ya vyuma chakavu, Je, Serikali haioni kwamba muda sasa umefika wa kupiga marufuku biashara hiyo hapa Zanzibar.

(b) Ni tani ngapi za bidhaa za chuma chakavu zimesafirishwa nje ya Zanzibar kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

7. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa kijiji cha Kajengwa wamekuwa wakipata tabu ya kukosa maji katika kijiji hicho. Kwa kuwa Serikali iliwaahidi wananchi hao kuwajengea tangi la maji ambalo hadi sasa bado halijajegwa.

Je, ni lini Serikali italijenga tangi la maji katika kijiji cha Kajengwa ili kuondoa kadhia ya kukosekana kwa maji katika kijiji hicho na vijiji jirani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

11. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Nchi za wenzetu kila siku zinazidi kupiga hatua za kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa biashara za matunda kama vile parachichi, zabibu na "apples".

Je, kwa hapa kwetu Zanzibar tumejipanga vipi kuwaelimisha wananchi wetu katika kilimo cha matunda hayo.

**Wizara ya Afya:**

52. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika maeneo mengi ya vijijini na yale yaliyo mbali na hospitali pamoja na vituo vya afya, wazazi wengi kabla kufikishwa vituo vya afya hulazimika kupata huduma ya wakunga wa kienyeji (Local Midwives) pale wanapojifungua. Kwa kuwa kumekuwa na matatizo mengi ya kiafya yanayoweza kumpata mzazi pamoja na mtoto ikiwa tahadhari kubwa haikuchukuliwa pale mzazi huyu anapohudumiwa na wakunga wa kienyeji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliondosha tatizo hilo.

(b) Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya ilishawahi kufanya tathmini ya Wakunga wa ngapi wa Kienyeji waliopo

Zanzibar.

(c) Je, pamoja na tatizo la kuwepo kwa wakunga wa kienyeji lakini bila ya shaka yoyote iwapo watapewa elimu bora, wataweza kuisaidia jamii zaidi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafunzo wakunga hao.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

14. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kipindi kirefu sasa kisiwani Pemba, kumejitokeza matukio ya mara kwa mara, kwa mabweni ya shule zetu kuungua moto hususan yale ya wanafunzi wetu wa kike.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara yako imeshafanya utafiti wowote kugundua vyanzo vya ajali hizi.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea mabweni ya wanafunzi wa kike tu kuungua moto na isiwe na yale ya wanaume.

(c) Je, Serikali kupitia Wizara yako imechukua hatua gani madhubuti za kuhakikisha ajali hizi hazitokei tena.

32. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Kisukari wamejenga chekechea ya jamii na mfadhili amewajengea madarasa manne ya ziada katika shehia ya Mtambwe kusini na wameomba usajili wa kudumu na bado hadi sasa hawajapatiwa.

Je, ni lini watapatiwa usajili wa kudumu.

## III. <u>KAULI YA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

(a) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali Kuu.
(b) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
(c) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma na Taasisi

zinazojitegemea.
(d) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi ya Miradi ya Maendeleo.
(e) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA.
(f) Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi Maalum (Special Audit).

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.

Zanzibar,
13 Septemba, 2022.